


# Tanzania

---



**Utafiti wa Afya ya Uzazi na  
Mtoto na Viashiria vya  
Malaria**

**2022**

**Ripoti ya Viashiria Muhimu**



## Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022

#### Ripoti ya Viashiria Muhimu

Wizara ya Afya  
Dodoma

Wizara ya Afya  
Zanzibar

Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Dodoma

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali  
Zanzibar

Programu ya DHS  
ICF  
Rockville, Maryland, USA

Januari 2023



Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (TDHS-MIS) ulitekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya. Utafiti wa TDHS-MIS umefadhiliwa na Serikali ya Tanzania, Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani (USAID); Mpango wa Rais wa Malaria (PMI), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Canada (CIDA); Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC); Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO); Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ); Hilton Foundation; Irish AID Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Nutrition International, Ubalozi wa Kifalme wa Norway; Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP). ICF Macro ilitoa msaada wa kiufundi kupitia programu inayofadhiliwa na Shirika la USAID lilitoa usaidizi wa kiufundi katika utekelezaji wa tafiti za kidemografia na afya katika nchi mbali mbali duniani.

Maelezo ya ziada kuhusu TDHS-MIS ya Mwaka 2022 yanaweza kupatikana kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi Kuu, Barabara ya Jakaya Kikwete, S. L. P 2683, Dodoma, Tanzania; simu: +255 26 - 2963822; nukushi: +255 26 – 2963828 ;barua pepe: sg@nbs.go.tz; Tovuti: www.nbs.go.tz.

Maelezo kuhusu programu ya DHS yanaweza kupatikana kutoka ICF Macro, 530 Gaither Road, Suite 500, Rockville, MD 20850, USA; simu: +1-301-407-6500; nukushi: +1-301-407-6501; barua pepe: info@DHSprogram.com; Tovuti: www.DHSprogram.com.

Maudhui yaliyomo katika ripoti hii ni jukumu la Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar, na ICF na si lazima yaakisi maoni ya USAID, Serikali ya Marekani, au mashirika mengine ya wafadhili.

Nukuu inayopendekezwa:

Wizara ya Afya (MoH) [Tanzania Bara], Wizara ya Afya (MoH) [Zanzibar], Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar, na ICF. *Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022. Ripoti ya Viashiria Muhimu*, Dodoma, Tanzania, na Rockville, Maryland, Marekani: MoH, NBS, OCGS, na ICF.



# YALIYOMO

---

MAJEDWALI NA VIELELEZO .....	vi
ACRONYMS AND ABBREVIATIONS .....	viii
DIBAJI ix	
VIASHIRIA VYA MALENGO ENDELEU YA DUNIA .....	x
UTANGULIZI.....	1
MALENGO YA UTAFIGI.....	2
UTEKELEZAJI WA UTAFIGI.....	3
MUUNDO WA SAMPULI .....	3
MADODOSO .....	5
UPIMAJI WA UREFU NA UZITO, UPUNGUFU WA DAMU NA MALARIA .....	7
VIPIMO VYA UZITO NA UREFU. ....	7
Upungufu wa damu. ....	7
Upimaji wa malaria kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo (RDT).....	8
Upimaji wa Upungufu wa madini joto.....	8
MAFUNZO YA WAKUFUNZI NA UTAFIGI WA MAJARIBIO .....	9
MAFUNZO YA WAFANYAKAZI WA UWANDANI .....	9
KAZI ZA UWANDANI.....	9
UCHAKATAJI WA TAARIFA .....	10
MATOKEO MUHIMU .....	10
KIWANGO CHA MWITIKIO.....	10
SIFA ZA WAHOJIWA.....	12
KIWANGO CHA UZAZI .....	15
KIWANGO CHA UZAZI KWA VIJANA .....	17
UHITAJI WA KUZAA WATOTO .....	20
UZAZI WA MPANGO.....	21
Matumizi ya Njia za uzazi wa Mpango .....	21
Mahitaji ya Uzazi wa mpango .....	26
VIFO VYA UTOTONI .....	30
HUDUMA YA AFYA YA UZAZI .....	32
Huduma Wakati wa Ujauzito.....	32
Chanjo ya pepopunda .....	33
Huduma wakati wa kujifungua .....	36
Huduma za uangalizi wa mama baada ya kujifungua .....	37
MODULI YA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO (ECDI 2030) .....	38
UTAFUTAJI WA HUDUMA NA MATIBABU YA MAGONJWA YA WATOTO.....	41
HALI YA LISHE KWA WATOTO .....	44

ULISHAJI WA WATOTO WACHANGA NA WADOGO .....	49
MALARIA .....	52
Umiliki na Matumizi ya Vyandarua Vyenye Dawa .....	52
Malaria wakati wa ujauzito .....	58
Huduma ya Matibabu ya Malaria kwa Watoto .....	60
Uthibiti wa Malaria kwa Watoto .....	62
VIRUSI VYA UKIMWI (VVU) na UKIMWI.....	65
Elimu ya kujikinga Miongoni mwa Vijana.....	65
Tabia za Kujamiiana .....	68
Huduma za mapema za Upimaji wa VVU .....	75
REJEA 81	

## MAJEDWALI NA VIELELEZO

Jedwali Na. 1: Matokeo ya Mahojiano ya Kaya na ya Mtu binafsi.....	11
Jedwali Na. 2: Sifa bainifu za wahojiwa.....	13
Jedwali Na. 3: Uwezo wa kuzaa kwa sasa.....	15
Jedwali Na. 4: Mimba za Utotoni.....	18
Jedwali Na .5: Uhitaji wa Kuzaa Watoto kwa Idadi ya Watoto Walio Hai .....	20
Jedwali Na. 6: Matumizi ya sasa ya njia za uzazi wa mpango kulingana na sifa Bainifu .....	22
Jedwali Na. 7: Haja na mahitaji ya uzazi wampango miongoni mwa wanawake walioolewa kwa sasa na wasioolewa lakini wanashiriki tendo la kujamiiana.....	27
Jedwali Na.8: Viwango vya Vifo vya utotoni .....	31
Jedwali Na. 9: Viashiria vya huduma za afya ya uzazi .....	34
Jedwali Na. 10: Malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto .....	39
Jedwali Na. 11 Matibabu kwa ajili ya maambukizi makali ya njia ya hewa, homa na kuharisha .....	42
Jedwali Na. 12: Hali ya lishe kwa watoto.....	46
Jedwali Na. 13: Viashiria vya njia bora za ulishaji watoto wachanga na watotowadogo (IYCF) .....	50
Jedwali Na. 14: Kaya zinazomiliki vyandarua vyenye dawa .....	53
Jedwali Na. 15: Matumizi ya vyandarua vyenye dawa kwa watoto na wanawake wajawazito .....	56
Jedwali Na.17: Watoto wenye homa na utafutaji wa huduma, uchunguzi namatibabu ya homa .....	60
Jedwali Na.18: Kiwango cha Malaria kwa Watoto .....	62

Jedwali Na.19: Elimu ya kujikinga na VVU Miongoni mwa Vijana .....	66
Jedwali Na. 20.1: Wanawake wenye wapenzi zaidi ya mmoja na uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa ya ngono katika kipindi cha miezi 12 iliyopita	69
Jedwali Na. 20.2: Wanaume wenye wapenzi zaidi ya mmoja na uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa ya ngono katika kipindi cha miezi 12 iliyopita	72
Jedwali Na. 21.1: Upatikanaji wa Huduma za mapema za Upimaji wa VVU kwa Wanawake .....	76
Jedwali Na. 21.2: Upatikanaji wa Huduma za mapema za Upimaji wa VVU kwa Wanaume .....	78

## **ORODHA YA VIELELEZO**

Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa uzazi kwa maeneo .....	16
Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa matumizi, haja ya mahitaji ya uzazi wa mpango ....	29
Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa vifo vya utotoni .....	31
Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa usaidizi wakati wa kujifungua .....	36
Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa hali ya lishe ya Watoto .....	45
Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa unyonyeshaji maziwa ya mama pekee .....	51
Kielelezo Na. 7: Mwenendo wa umiliki wa vyandarua vilivyowekwa dawa .....	54
Kielelezo Na. 8 : Mwenendo wa kiwango cha malaria kwa Watoto .....	64

## ACRONYMS AND ABBREVIATIONS

ADDO	Accredited Drug Dispensing Outlet
ACT	Artemisinin-Based Combination Therapy
ANC	Antenatal Care
ARI	Acute Respiratory Infection
CAPI	Computer-Assisted Personal Interviewing
CBR	Crude Birth Rate
CDC	Centers for Disease Control and Prevention
CIDA	Canadian International Development Agency
CSPRO	Census and Survey Processing
DHS	Demographic and Health Survey
EA	Enumeration Area
ECDI2030	Early Childhood Development Index 2030
FCDO	Foreign, Commonwealth and Development Office
GFR	General Fertility Rate
GIZ	Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit
IPTp	Intermittent Preventive Treatment During Pregnancy
IRB	Internal Review Board
ITN	Insecticide-Treated Net
IUD	Intrauterine Contraceptive Device
IYCF	Infant and Young Child Feeding
LAM	Lactational Amenorrhea Method
LHRC	Legal and Human Rights Centre
LLIN	Long-lasting Insecticidal Net
MCH	Maternal and Child Health
MoH	Ministry of Health (Zanzibar)
WAMJW	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
VVU	Virusi Vya Ukimwi
NBS	National Bureau of Statistics
NGO/VCT	Non-governmental organisation/Voluntary Counselling and Testing
OCGS	Office of the Chief Government Statistician
ORS	Oral Rehydration Salts
PMI	President's Malaria Initiative
PNC	Postnatal Care
RDT	Rapid Diagnostic Test
SD	Standard Deviation
SDG	Sustainable Development Goal
SDM	Standard Days Method
SP	Sulfadoxine-Pyrimethamine
TDHS-MIS	Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey
TFR	Total Fertility Rate
TFNC	Tanzania Food and Nutrition Centre
UNICEF	United Nations Children's Fund
USAID	United States Agency for International Development
WFP	World Food Programme
WHO	World Health Organization



## DIBAJI

Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (TDHS-MIS) ni utafiti wa Saba (7) kufanyika nchini Tanzaniakupitia programu ya DHS. Utafiti wa TDHS/MIS wa Mwaka 2022 ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), Zanzibar na Wizara za Afya (MOH) kutoka Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia; Wanawake na Makundi Maalum (WAMJW); Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC); Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC); Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Lengo kuu la Utafiti wa TDHS/MIS wa Mwaka 2022 ni kupata taarifa za sasa za afya na takwimu zinazohusiana na masuala ya afya ili kusaidia kuboresha sera katika ajenda ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa:- Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/22 - 2025/26), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26, Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050 (EAC 2050), Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 (ADA 2063) na Ajenda ya Kimataifa ya 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030) na kutathmini hatua iliyofikiwa katika kuboresha hali ya maisha ya watu nchini. Ripoti hii inawasilisha Viashiria Muhimu kutoka TDHS/MIS ya Mwaka 2022; ripoti ya kina zaidi itachapishwa Juni, Mwaka 2023.

TDHS/MIS ya Mwaka 2022 ilihusisha wadau wengi, ikijumuisha; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ICF Macro International; Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani(USAID); Serikali ya Uingereza; Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Canada (CIDA); the Centers for Disease Control and Prevention (CDC); the Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO); Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ); Hilton Foundation; Irish AID, Nutrition International; Ubalozzi wa Kifalme wa Norway; Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Bill and Melinda Gates Foundation.

Ni matumaini yangu kwamba, Ripoti hii ya viashiria muhimu itawawezesha watunga sera, mameneja wa programu mbalimbali na wadau wengine kupata taarifa muhimu wanazohitaji katika utekelezaji wa majukumu yao wakati wakisubiri Ripoti ya kina ya Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022.

**Umyy A. Mwalimu (Mb.)**

Waziri wa Afya

# VIASHIRIA VYA MALENGO ENDELEU YA DUNIA

## Viashiria vya Malengo Endelevu ya Dunia Vitakavyopimwa —Tanzania DHS-MIS 2022

Kiashiria	Jinsi		Jumla
	Wanaume	Wanawake	
<b>2. LENGO NAMBA MBILI - Kutokomeza Njaa, Kuwa na Uhakika wa Chakula, Lishe Bora na Kukuza Kilimo Endelevu</b>			
<b>2.2.1 Asilimia ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 ambao wamedumaa</b>	33.3	26.6	30.0
<b>2.2.2 Asilimia ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 ambao wana utapiamlo</b>			
<b>a) Asilimia ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 ambao wakondefu</b>	4.2	2.4	3.3
<b>b) Asilimia ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 ambao wana uzito uliozidi</b>	3.7	3.3	3.5
<b>3. LENGO NAMBA TATU - Kuhakikisha Afya Njema na Ustawi wa Watu wa Rika Zote</b>			
<b>3.1.2 Asilimia ya watoto waliozaliwa kwa msaada wa mtoa huduma ya afya mwenye ujuzi</b>	na	na	85.0
<b>3.2.1 Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka 5<sup>1</sup></b>	na	na	43.0
<b>3.2.2 Vifo vya watoto wachanga kabla ya kutimiza mwezi mmoja<sup>1</sup></b>	na	na	24.0
<b>3.7.1 Asilimia ya wanawake wenye umri wa kuzaa (miaka 15-49) ambao mahitaji yao ya njia za uzazi wa mpango za kisasa yamefikwa.</b>	na	53.1	na
<b>3.7.2 Kiwango cha mimba za utotoni kwa kila wanawake 1,000</b>			
<b>c) Wasichana wenye umri wa miaka 10-14<sup>2</sup></b>	na	1	na
<b>d) Wanawake wenye umri wa miaka 15-19<sup>3</sup></b>	na	112	na
<b>4. LENGO NAMBA NNE - Kuhakikisha Elimu Bora, Yenye Usawa na Kutoa Fursa kwa Wote Kujiendeleza</b>			
<b>4.2.1 Asilimia ya watoto wenye umri wa miezi 24–59 ambao wana maendeleo katika hali ya afya, ujifunzaji na ustawi wa kisaikolojia, kwa jinsia<sup>4</sup></b>	44.1	50.8	47.4

na = Haihusiki

<sup>1</sup>Hukokotolewa kwa kuzingatia vifo vya watoto kati ya vizazi hai 1,000 katika kipindi cha miaka mitano kabla ya utafiti

<sup>2</sup> Ni sawasawa na kiwango cha uzazi kwa umri maalum kwa wasichana wenye umri wa miaka 10-14 katika kipindi cha miaka 3 kabla ya utafiti, hukokotolewa kwa kuzingatia vizazi hai 1,000 kwa wasichana wenye umri wa miaka 10-14

<sup>3</sup>Ni sawasawa na kiwango cha uzazi kwa umri maalum kwa wasichana wenye umri wa miaka 15-19 katika kipindi cha miaka 3 kabla ya utafiti, hukokotolewa kwa kuzingatia vizazi hai 1,000 kwa wasichana wenye umri wa miaka 15-19

<sup>4</sup> Ni sawasawa na fahirisi ya maendeleo ya ukuaji wa mtoto katika hali ya afya, ujifunzaji na ustawi wa kisaikolojia (ECDI 2030).

# TANZANIA



Mgawanyo wa Mikoa Kikanda Kulingana na Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022.

## UTANGULIZI

Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (TDHS-MIS) ulitekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afyana Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC). Ukusanyaji wa taarifa za Utafiti huu ulianza mwezi Februari na kukamilika mwezi Julai 2022.

Shirika la ICF lilitoa msaada wa kitaalamu kupitia programu ya Utafiti wa Afya ya Uzazi (DHS), ambayo inatoa msaada wa kifedha na wa kitaalamu katika tafiti za idadi ya watu na afya katika nchi mbalimbali duniani kwa ufadhili wa Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani (USAID). Shukrani za kipekee ziende kwa Taasisi na Washirika wa Maendeleo wakiwemo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Mpango wa Rais wa Kupambana na Malaria (PMI); Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Canada (CIDA); Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC); Ofisi ya Mahusiano, Jumuiya ya Madola na Maendeleo (FCDO); the Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ); Hilton Foundation; Irish AID; Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC); Shirika la Kimataifa la Lishe (NI); Ubalozi wa Kifalme wa Norway na waliofanikisha utekelezaji wa Utafiti huu kwa msaada wa kitaalamu na kifedha.

Ripoti hii ya Viashiria Muhimu inatoa baadhi ya matokeo ya viashiria vichache muhimu vilivyochaguliwa kutoka Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya Utafiti huu utawasilishwa katika ripoti itakayotolewa kuu katika robo ya pili ya mwaka 2023.

## MALENGO YA UTAFITI

- a) Kukusanya taarifa ili ziweze kukokotoa viashiria mbalimbali vya kidemografia ikiwa ni pamoja kiwango cha uzazi, kiwango cha vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja na wenye umri chini ya miaka 5, viwango vya vifo kwa watu wazima na vifo vitokanavyo na uzazi.
- b) Kukusanya taarifa za ulemavu miongoni mwa wanakaya;
- c) Kupima kiwango cha uelewa na matumizi ya njia za uzazi wa mpango;
- d) Kukusanya taarifa zinazohusiana na uzazi, uwezo wa kuzaa, uwezo wa kupanga idadi ya watoto wanaopenda kuzaa maishani na mahiitaji yasiyotimizwa ya njia za uzazi wa mpango;
- e) Kukusanya taarifa kuhusu afya ya uzazi kwa wanawake (wajawazito, wanaojifungua, na huduma baada ya kujifungua) afya na lishe ya watoto (kunyonyesha na vyakula vya ziada, chanjo, uwepo wa magonjwa ya utotoni na matibabu yake);
- f) Kukusanya taarifa za matumizi ya vyandarua vilivyowekwa dawa, watu waliolala kwenye vyandarua na matumizi ya dawa za malaria kwa ajili ya kutibu homa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5;
- g) Kukusanya taarifa kutoka kwa wanawake kuhusu matukio ya unyanyasaji kwa wanawake majumbani (unyanyasaji wa kijinsia, kimwili na kingono);
- h) Kukusanya taarifa za vifo vitokanavyo na uzazi, na vifo vya watu wazima kwa kuwauliza ndugu wa kuzaliwa naye yaani kaka na dada zake (*sisterhood method*);
- i) Kukusanya taarifa kuhusu ukeketaji miongoni mwa wanawake wanaostahili kuhojiwa wenye umri wa miaka 15–49;
- j) Kutathmini hali ya lishe ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, na wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-49, kwa kutumia vipimo vya urefu na uzito na kupima upungufu wa damu kati ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 na watoto chini ya miaka 5;
- k) Kupata makisio ya kiwango cha maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto wa miezi 6-59 kulingana na vipimo vya uchunguzi wa papo kwa papo,
- l) Kutoa taarifa juu ya kuenea kwa shinikizo la damu miongoni mwa watu wazima
- m) Kupima hali ya virutubishi kwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 na watoto wenye umri wa miezi 6-59 kupitia kuchukua sampuli ya damu iliyochukuliwa kutoka kwenye mishipa ya damu.

Taarifa zilizokusanywa katika Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 zinategemewa kuwasaidia watunga sera na wasimamizi wa programu kuandaa na kutathmini programu pamoja na mikakati ya kuboresha afya kwa Watanzania. Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 pia unatoa viashiria muhimu vya kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa Tanzania na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 (FYDP-III).

## UTEKELEZAJI WA UTAFITI

### MUUNDO WA SAMPULI

Sampuli ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 ilipatikana katika hatua mbili na ilifanyika ili kutoa makadirio ya viashiria kwa Nchi nzima, maeneo ya Mijini na Vijijini kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa viashiria mahususi, kama vile matumizi ya njia za uzazi wa mpango, sampuli ya Utafiti huu inaruhusu kutoa makadirio ya viashiria hivyo mkoa kwa mikoa yote 31 ya Tanzania – ikiwa ni Mikoa 26 kwa Tanzania Bara na Mikoa 5 kwa Zanzibar. Hatua ya kwanza, ilihusisha uchaguzi wa Maeneo ya Utafiti (Clusters) ambayo ni Maeneo ya Kuhesabia Watu (EAs) yalitokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Jumla ya maeneo ya kuhesabia watu 629 yalichaguliwa katika hatua ya kwanza. Kati ya maeneo hayo, maeneo ya kuhesabia watu 211 yalikuwa ni ya Mijini na 418 ya Vijijini.

Katika hatua ya pili, kaya 26 zilichaguliwa kitaalam kutoka kwenye kila eneo la utafiti, kuwezesha upatikanaji wa sampuli ya kaya wakilishi 16,354 zitakazoshiriki katika Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022.

Zoezi la kuorodhesha kaya katika maeneo yote ya Utafiti yaliyochaguliwa lilifanyika kabla ya kuanza kwa zoezi kuu la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti huu. Zoezi la kuorodhesha kaya lilihusisha kutembelea kila eneo lililochaguliwa kwa ajili ya utafiti, kuchora ramani inayoelekeza namna ya kufika kwenye eneo la utafiti, kuchora ramani yenye kuonyesha vielelezo vinavyopatikana katika eneo la utafiti, kuorodhesha kaya binafsi zinazopatikana katika eneo la utafiti hii ikiwa ni pamoja na anuani za majengo na majina ya wakuu wa kaya. Orodha ya kaya iliyopatikana kutokana na zoezi la kuorodhesha kaya ilitumika a katika hatua ya pili ambayo ilikuwa ni kuchagua kayazitakazoshiriki katika utafiti. Wakati wa zoezi la kuorodhesha kaya, timu ya uwandani ilikusanya taarifa za majira nukta (GPS) kwa kila kila eneo la kuhesabia watu.

Kwa madhumuni ya Utafiti huu, Tanzania iligawanywa katika Kanda tisa (9) ili kuweza kutoa makadirio ya viashiria vya kidemografia yatakayoonesha utofauti katika ngazi ya kanda. Ingawa kanda hizi rasmi sio rasmi katika muundo wa kiutawala, zimekuwa zikitumiwa na Kitengo cha Afya ya Uzazi na Mtoto cha Wizara ya Afya. Uunganishaji wa mikoa katika kuunda kanda, umewezesha uwepo idadi kubwa ya watu katika ukokotoaji wa viashiria mbali mbali kwa ngazi ya kanda. Mchanganuo wa kanda hizo ni kama ifuatavyo:

- a) **Kanda ya Magharibi:** Tabora na Kigoma
- b) **Kanda ya Kaskazini:** Kilimanjaro, Tanga na Arusha
- c) **Kanda ya Kati:** Dodoma, Singida na Manyara
- d) **Nyanda za Juu Kusini:** Iringa, Njombe na Ruvuma
- e) **Kanda ya Kusini:** Lindi na Mtwara
- f) **Nyanda za Juu Kusini-Magharibi:** Mbeya, Rukwa, Katavi na Songwe
- g) **Kanda ya Ziwa:** Kagera, Mwanza, Geita, Mara, Simiyu na Shinyanga
- h) **Kanda ya Mashariki :** Dar es Salaam, Pwani na Morogoro
- i) **Kanda ya Zanzibar:** Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini Magharibi, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

Wanawake wote wenye umri wa miaka 15–49 ambao walikuwa ni wakazi wa kawaida katika kaya au walikuwa ni wageni ambao walilala kwenye kaya usiku wa kuamkia siku ya mahojiano walijumuishwa katika Utafiti huu na walistahili kuhojiwa. Katika sampuli ndogo ambayo ni asilimia 50 ya kaya zote zilizochaguliwa, wanaume wote wenye umri wa miaka 15–49 walistahili kuhojiwa iwapo walikuwa ni wakazi wa kawaida katika kaya au walikuwa ni wageni ambao walilala kwenye kaya usiku wa kuamkia siku ya mahojiano. Katika sampuli hii ndogo ambayo ni asilimia 50 ya kaya zote zilizochaguliwa, watoto wote wenye umri wa miezi 0–59 (kwa idhini au ruhusa ya mzazi au mlezi), wanawake wote wenye umri wa miaka 15–49, na wanaume wote wenye umri wa miaka 15–49 walipimwa urefu na uzito. Vile vile, watoto wenye umri wa miezi 6–59 walipimwa upungufu wa damu na malaria kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo. Wanawake wenye umri wa miaka 15–49 walipimwa upungufu wa damu na waliombwa idhini ya kutoa sampuli ya mkojo uliopelekwa maabara kwa ajili ya kupima uwepo wa madini joto mwilini.

Sampuli ndogo ambayo ni takriban asilimia 20 ya kaya zote zilizochaguliwa zilishiriki kwa ajili ya moduli ya kupima virutubishi. Katika kaya hizo, wanawake wote wenye umri wa miaka 15-49 waliohojiwa na watoto wote wenye umri wa miezi 6-59 walistahili kuchukuliwa sampuli ya damu kutoka kwenye mishipa ya damu. Sampuli hizi zilikusanywa, kuchambuliwa na zilipelekwa kwenye Maabara ya Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kwa ajili ya kuzihifadhi na kufanya uchunguzi. Matone ya damu kutoka kwenye mishipa ya damu kutoka kwa wanawake na watoto yalitumika kupima upungufu wa damu na malaria huko uwandani kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo (RDT). Uchunguzi mbali mbali unaohusiana na moduli ya virutubishi utafanywa na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) na matokeo yake yatatolewa katika chapisho tofauti kwa siku zijazo.



## MADODOSO

Madodoso ya aina nne yalitumika katika Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022: Dodoso la Kaya, Dodoso la Mwanamke, Dodoso la Mwanaume, na Dodoso la Vipimo (Biomarker). Kulingana na programu ya muundo wa Madodoso ya DHS, madodoso hayo yalihuishwa ili kuakisi hali halisi ya kidemografia na masuala ya afya ya Tanzania. Aidha, kulikuwa na dodoso la ziada lililokusanya taarifa kuhusu wafanyakazi walioshiriki katika zoezi la ukusanyaji wa taarifa za utafiti huu huko uwandani.

Dodoso la Kaya lilitumika kuorodhesha wanakaya wa kawaida na wageni wote katika kaya zilizochaguliwa. Taarifa za msingi za kidemografia katika kaya zilikusanywa kwa kuangalia taarifa za kila mtu aliyeorodheshwa, ikijumuisha umri, jinsi, hali ya ndoa, elimu, na uhusiano wa kila mmoja na mkuu wa kaya. Hali ya uhai wa wazazi ilibainishwa kwa watoto waliokuwa na umri chini ya umri wa miaka 18. Taarifa kuhusu umri na jinsi ya wanakaya iliyopatikana katika Dodoso la Kaya ilitumiwa kutambua wanawake na wanaume ambao walistahili kuingia katika mahojiano ya mtu binafsi. Dodoso la Kaya pia lilikusanya taarifa kuhusu makazi ya kaya, kama vile chanzo cha maji, aina ya vyoo, vifaa vilivyotumika kusakafia nyumba, umiliki wa vifaa mbalimbali, umiliki na matumizi ya vyandarua. Maswali machache katika Dodoso la Kaya yaliulizwa kuhusu hali ya ulemavu ya wanakaya wenye umri wa miaka mitano au zaidi.

Dodoso la Mwanamke lilitumika kukusanya taarifa kutoka kwa wanawake wote wanaostahili kuhojiwa (umri wa miaka 15–49). wanawake hawa waliombwa kutoa taarifa zifuatazo:

- a) Sifa bainifu za mhojiwa (umri, elimu, uelewa kuhusu kupata taarifa kupitia vyombo vya habari, na kadhalika);
- b) Historia ya uzazi na vifo vya watoto;
- c) Uelewa na matumizi ya njia za uzazi wa mpango;
- d) Upendeleo wa kuzaa;
- e) Huduma wakati wa ujauzito, kujifungua na baada ya kujifungua;
- f) Kunyonyesha na kulisha watoto wachanga;
- g) Chanjo na magonjwa ya watoto;
- h) Ndoa na tendo la kujamiiana;
- i) Kazi ya mwanamke na sifa bainifu za mume;
- j) Masuala mengine ya afya;
- k) Kiwango cha vifo kwa watu wazima, pamoja na vifo vitokanavyo na uzazi;
- l) Ukeketaji;
- m) Makuzi na Maendeleo ya watoto;
- n) Malaria na
- o) Ukatili wa majumbani

Dodoso la Mwanaume lilitumika kukusanya taarifa za wanaume wote wenye umri wa miaka 15–49 katika sampuli ndogo ya kaya zilizochaguliwa kwa mahojiano ya wanaume. Dodoso la Mwanaume lilikusanya taarifa karibu sawa na zilizopatikana katika Dodoso la Mwanamke, lakini lilikuwa fupi kwa sababu halikuwa na taarifa za kina kuhusu historia ya uzazi au maswali juu ya afya ya mama na mtoto.

Dodoso la Vipimo (Biomarker) lilitumika kukusanya taarifa za vipimo vya urefu na uzito kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 na wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-49; kukusanya matokeo ya uchunguzi wa upungufu wa damu kwa watoto wenye umri wa miezi 6-59 na wanawake wenye umri wa miaka 15-49; kukusanya taarifa za matokeo ya uchunguzi wa malaria kwa watoto wa miezi 6-59 kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo; na kuandika iwapo idhini ya kuchukua sampuli ya chumvi katika kaya na sampuli ya mkojo



miongoni mwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 imetolewa. Sampuli za mkojo zilipaswa zitapimwa katika maabara ya TFNC kwa ajili ya kubaini uwepo wa madini joto mwilini.

Dodoso la Mfanyakazi wa Uwandani lilikusanya taarifa za msingi za wafanyakazi hao na lilijumuisha wasimamizi wa timu, wasimamizi wa programu ya CAPI, Wadadisi, na Wataalamu wa vipimo.

Madodoso na andiko la utafiti, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa madodoso na ukusanyaji wa vipimo, ziliidhinishwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu Tanzania Bara (NIMRI) na Taasisi ya Utafiti wa Afya ya Zanzibar (ZAHRI) na kukaguliwa na Bodi ya Ukaguzi wa Ndani (IRB) ya ICF.

## UPIMAJI WA UREFU NA UZITO, UPUNGUFU WA DAMU NA MALARIA

### VIIMO VYA UZITO NA UREFU.

Vipimo vya uzito vilichukuliwa kwa kutumia mizani aina ya *Seca* (namba ya muundo SECA 878U). Vipimo vya urefu vilipimwa kwa ubao maalum wa kupimia unaoitwa *ShorrBoard*. Watoto walio na umri wa chini ya miezi 24 walipimwa urefu wakiwa wamelazwa juu ya ubao chini, wakati watoto wakubwa na watu wazima walipimwa wakiwa wamesimama.

Ili kutathmini usahihi wa vipimo, watoto wawili kwa kila eneo la utafiti walichaguliwa bila mpangilio ili kupimwa kwa mara ya pili. Programu ya DHS inafafanua tofauti ya chini ya sentimita 1 kati ya vipimo viwili vya urefu kama kiwango kinachokubalika cha usahihi. Watoto walio na kiwango cha juu cha udumavu, ukondefu na wenye uzito mdogo kupita kiasi unaopimwa kwa kiwango cha chini cha kipimo ( $zscore-3$ ) au kiwango cha juu cha kipimo ( $zscore+3$ ) walilazimika kurudiwa kupimwa kwa mara ya pili. Upimaji wa mara ya pili ulihakikisha ubora wa vipimo vya urefu na uzito uliopatikana.

Watoto waliothibitika kuwa na kiwango cha juu cha udumavu, ukondefu na wenye uzito mdogo kupita kiasi kwa kutumia kiwango cha chini cha kipimo ( $zscore-3$ ) au kiwango cha juu cha kipimo ( $zscore+3$ ) walipewa rufaa kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi zaidi.

### UPUNGUFU WA DAMU.

Vielelezo vya sampuli ya damu kwa ajili ya kupima upungufu wa damu vilikusanywa kutoka kwa wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-49 ambao walikubali kupimwa. Sampuli za damu pia zilikusanywa kutoka kwa watoto wenye umri wa miezi 6-59 ambao wazazi au walezi wao walikuwa wametoa idhini ya kupimwa. Sampuli za damu zilitolewa kutokana na damu iliyochukuliwa kutoka kwenye kidole (au kweye kisigino) kwa watoto wenye umri wa miezi 6-11 na kukusanywa katika kifaa maalum kinachoitwa *microcuvette*. Uchunguzi wa chembe hai nyekundu za damu (*hemoglobin*) ulifanyika kwenye kaya husika kwa kutumia kifaa kinachofanya kazi kwa kutumia betri kiitaalam kinaitwa *HemoCue201+*. Kwa wale waliofanyiwa vipimo matokeo yalitolewa papo kwa papo kwa njia ya mdomo na maandishi. Wazazi au walezi wa watoto wenye kiwango cha hemoglobin chini ya 8 g/dl walipewa rufaa kwa kuelekezwa kumpeleka mtoto katika kituo cha kutolea huduma za afya kwa ajili ya ufuatiliaji. Watu wazima nao pia walipewa rufaa kwa ajili ya ufuatiliaji ikiwa viwango vyao vya hemoglobini vilikuwa chini ya 8 g/dl.

---

## **UPIMAJI WA MALARIA KWA KUTUMIA KIPIMO CHA PAPO KWA PAPO (RDT).**

Lengo lingine kuu la Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 lilikuwa ni kutoa taarifa kuhusu kiwango cha maambukizi ya malaria miongoni mwa watoto wenye umri wa miezi 6-59. Kwa kutumia kidole au kisigino kilichotumika kutoa tone la damu kwa ajili ya kupima upungufu wa damu, tone la damu lilitumika kupima malaria kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo (*SDBiolineAg Pf RDT*), ambacho ni kipimo maalum cha kupima *Plasmodium falciparum (Pf)* ambacho ni kisababishi kikubwa cha malaria Tanzania. Kipimo hicho kinajumuisha sample applicator iliyofungashwa kwenye paketi maalum na huwa inatumika mara moja tu na kutupwa. Tone dogo la damu huwa linaingizwa kwenye hiyo sample applicator na kisha kuwekwa kwenye hicho kifaa cha kupimia (SD BiolineAg Pf RDT. Wataalamu wa kuchukua vipimo walifundishwa namna ya kupima malaria kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo uwandani, kwa kuzingatia maelekezo ya watengenezaji wa vifaa hivyo. Kama ilivyo kwa upimaji wa upungufu wa damu, matokeo ya malaria kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo yalitolewa kwa mzazi au mlezi wa mtoto kwa njia ya mdomo na maandishi na pia yalijazwa kwenye dodoso la vipimo.

Watoto waliopimwa na kukutwa na malaria kwa kutumia kipimo cha papo kwa papo walipatiwa matibabu kamili kwa mujibu wa miongozo ya kitaifa ya matibabu ya malaria nchini Tanzania, kama kwa wakati huo hawakuwa wakitumia dawa ya mseto (ACT) kwa ajili ya kutibu malaria na kama walikuwa hawajatumia dozi kamili ya dawa hiyo wiki 2 kabla ya Utafiti. Ili kujua kipimo sahihi cha kutoa matibabu ya malaria, wataalamu wa vipimo walipewa chati zinazotoa miongozo na maelekezo ya namna ya kutibu malaria na walielekezwa kuuliza kama mtoto alikuwa na dalili hatarishi za malaria na pia kuulizia kama mtoto alikuwa anatumia dawa zozote za kutibu malaria. Wataalamu wa maabara/wauguzi walitoa dozi sahihi ya dawa ya mseto inayoendana na umri wa mtoto na kuwapa wazazi/walezi maelekezo ya jinsi ya kuwapatia dawa watoto hao. Watoto waliokutwa na malaria na kuonyesha dalili hatarishi za malaria- kuwa kiwango kidogo cha damu chini ya 8 g/dl, udhaifu mkubwa, kupoteza fahamu, kupumua kwa haraka, degedege, kutokwa na damu, homa ya manjano na kutoa mkojo mweusi - hawakupewa matibabu. Kwa vile matibabu ya hatua ya kwanza ya malaria kali ni dawa ya kwini (parenteral quinine), wazazi au walezi walishauriwa kumpeleka mtoto kwenye kituo cha kutolea huduma za afya mara moja. Wazazi au walezi wa watoto wengine wote waliotibiwa waliambiwa wawapeleke watoto wao kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mara moja ikiwa wataendelea kuugua, watapata homa au kushindwa kupumua, au watashindwa kunywa maji au kunyonya. Kulingana na taratibu za sasa za kutokomeza malaria Zanzibar wazazi pia walipewa ushauri nasaha kuhusu jinsi ya kuzuia malaria. Watoto waliogundulika kuwa na ugonjwa wa Malaria kwa upande wa Zanzibar hawakutibiwa bali walipewa rufaa kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo karibu zaidi kwa kuzingatia.

---

## **UPIMAJI WA UPUNGUFU WA MADINI JOTO.**

Timu za mahojiano ziliwaomba wanawake katika kaya zilizochaguliwa watoe sampuli za mikojo zilizopelekwa maabara kwa ajili ya kupima uwepo wa madini joto mwilini. Sampuli za mikojo zilizokusanywa ziliwekwa kwenye vichupa vidogo vyenye mifuniko iliyofungwa vizuri kwa ajili ya kusafirishwa kwenda maabara ya TFNC. Majibu ya vipimo vya upungufu wa damu na madini joto yatatolewa katika ripoti tofauti wakati wa kutoa matokeo ya ripoti za Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022.

## **MAFUNZO YA WAKUFUNZI NA UTAFITI WA MAJARIBIO**

Utafiti wa majaribio ulifanyika mkoani Kilimanjaro kuanzia tarehe 30 Septemba hadi tarehe 21 Oktoba 2021. Jumla ya wadadisi 18 (wanawake 12 na wanaume 6) na wataalamu wa afya 6 (wanaume 3 na wanawake 3) walishiriki katika mafunzo hayo yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) na Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka shirika la ICF. Mafunzo ya darasani yalifanyika katika siku 15 za mwanzo, na kazi ya uwandani yalifanyika kwa siku 4 katika maeneo mawili ya utafiti ya vijijini na eneo moja la mjini. Kufuatia mazoezi ya uwandani, kikao cha kujadili tathmini ya kazi kilifanyika kwa pamoja na wafanyakazi walioshiriki utafiti wa majaribio. Marekebisho ya dodoso pamoja na programu ya kompyuta (CAPI) yalifanyika kulingana na majadiliano yaliyotokana na zoezi hilo.

Mafunzo ya wakufunzi wa maudhui ya dodoso na mfumo wa CAPI yalifanyika kabla ya mafunzo ya Wasimamizi na Wadadisi kuanzia tarehe 19 Januari hadi 25 Januari 2022 mjini Moshi mkoani Kilimanjaro.

## **MAFUNZO YA WAFANYAKAZI WA UWANDANI**

Mafunzo ya Wasimamizi na Wadadisi ya Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 yalifanyika mkoani Kilimanjaro kuanzia tarehe 26 Januari 2022 hadi tarehe 21 Februari 2022. Jumla ya wadadisi 120 kutoka katika mikoa mbalimbali hapa nchini - wauguzi wanawake 60, wauguzi wanaume 20, viongozi wa timu 20 na wasimamizi wa programu ya CAPI 20 - walishiriki katika mafunzo hayo. Mafunzo hayo yaliendeshwa na wakufunzi kutoka NBS, OCGS, TFNC, NMCP na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka ICF. Kwa kushirikiana na ICF, wakufunzi kutoka TFNC na UNICEF walitoa mafunzo kwa wataalamu wa vipimo 80 (wataalamu 40 waliofundishwa kuchukua vipimo vya kawaida vya viashiria lishe (Standard Biomarkers) na wataalamu 40 waliofundishwa kuchukua vipimo vya virutubishi (Micronutrients Biomarkers)).

Washiriki walipimwa uwezo wao kupitia mazoezi ya darasani, maswali, na uangalizi uliofanywa wakati wa mazoezi ya uwandani. Hadi kufikia mwisho wa mafunzo hayo, timu 18 ziliundwa, zilijumuisha viongozi wa timu 18, wasimamizi wa CAPI 18, wadadisi wanaume 18, wadadisi wa kike 54, wataalamu 36 wa vipimo vya kawaida vya viashiria lishe (Standard Biomarkers) na wataalamu 36 wa vipimo vya virutubishi (Micronutrients Biomarkers). Wadadisi wote walikuwa ni wauguzi. Viongozi wa timu na wasimamizi wa CAPI walipata mafunzo ya ziada ya namna ya kuzitambua kaya zilizochaguliwa; jinsi ya kutambua kaya na watu waliohusika katika sampuli ndogo ya utafiti, kuratibu na kudhibiti ubora wa taarifa zilizokusanywa; na jinsi ya kuratibu kazi za uwandani.

Wataalamu wote wa vipimo vya kawaida vya viashiria lishe walikuwa wauguzi, na walifundishwa jinsi ya kupima urefu na uzito wa watoto na watu wazima. Mafunzo juu ya uchukuaji wa kipimo cha urefu kwa mtoto yalijumuisha mazoezi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa, na mazoezi haya yalirudiwa kwa wale wataalamu ambao hawakuweza kufikia viwango vinavyohitajika vya uelewa.

## **KAZI ZA UWANDANI**

Ukusanyaji wa taarifa za Utafiti huu ulifanywa na timu 18, timu 3 zilifanya kazi Zanzibar na timu 15 zilifanya kazi Tanzania Bara. Kila timu ilipewa magari wawili na madereva wawili. Timu hizo zilijumuisha msimamizi wa timu, msimamizi wa CAPI, wadadisi watatu wa kike, mdadisi mmoja wa kiume, wataalamu wa vipimo vya kawaida vya viashiria lishe wawili na wataalamu wa vipimo vya virutubishi wawili.

Msimamizi wa timu na msimamizi wa programu ya CAPI waliwajibika kuhakikisha ubora wa taarifa zinazokusanywa uwandani. NBS, OCGS na TFNC ziliratibu na kusimamia shughuli zote za uwandani. Shirika la ICF lilitoa msaada wa kiufundi katika kipindi chote cha miezi 5 cha kukusanya taarifa za utafiti huu. Kazi ya ukusanyaji wa taarifa za utafiti huu ilianza tarehe 24 Februari, 2022 na kukamilika tarehe 21 Julai, 2022.

Ufuatiliaji wa kazi za uwandani ulikuwa ni sehemu muhimu ya Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 na ulifanyika katika kipindi cha ukusanyaji wa taarifa. Kazi hii ilifanywa na NBS, OCGS, TFNC, NMCP na ICF. Majedwali ya kuangalia mwenendo wa kazi yalitolewa mara kwa mara kutoka kwenye mfumo wa kielektroniki wa "syncloud" ili kufuatilia ubora wa taarifa zilizokuwa zinakusanywa na maendeleo ya kazi za uwandani. Timu zilipewa mrejesho wa mara kwa mara ili kuboresha ubora wa taarifa na kuendeleza ufanisi mzuri katika kazi.

## UCHAKATAJI WA TAARIFA

Uchakataji wa taarifa za Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 ulianza mara tu baada ya kuanza kwa zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti huu. Mara baada ya kukamilisha ukusanyaji wa taarifa kwenye eneo la utafiti, taarifa hizo zilitumwa kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia teknolojia ya "Syncloud" kwenda kwenye mfumo wa kuhifadhi taarifa uliowekwa katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Dodoma. Taarifa hizo zilipokelewa na kuchakatwa na kuhaririwa ili kuweza kuangalia iwapo kuna taarifa zinazokinzana, taarifa ambazo hazijakamilika au taarifa ambazo zisizoendana na hali iliyopo. Ilipoonekana taarifa zilizokusanywa zina makosa au zinakinzana mrejesho wa makosa hayo uliwasilishwa kwa timu husika ili yaweze kusahihishwa. Uhariri wa kazi kwa hatua ya pili iliofanywa na watalaam kutoka NBS na OCGS wakishirikiana na wasimamizi wa timu zilizokuwa uwandani ulifanyika katika ofisi za NBS Makao Makuu Dodoma, ulijumuisha kuweka mageresho kwa majibu ya maswali ambayo hayakuwa na mageresho na kutatua tatizo la taarifa zilizokuwa zinakinzana. Madodoso ya vipimo yaliyokuwa katika mfumo wa karatasi kutoka uwandani yalisafirishwa kwenda Ofisi ya Taifa ya Takwimu na taarifa zilizokusanywa kwa mfumo huo wa karatasi zililinganishwa na taarifa za namna hiyo zilizokusanywa kwa mfumo wa kielektroniki ili kuweza kuangalia usahihi na ubora wa taarifa hizo. Uchakataji na uhariri wa taarifa ulifanywa kwa kutumia programu ya CSPPro. Kufanyika kwa zoezi la uchakataji wa taarifa za Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 ulioenda sambamba na zoezi la ukusanyaji wa taarifa za utafiti huu ulikuwa na msaada mkubwa katika kupunguza uwezekano wa kufanya makosa katika taarifa zilizokusanywa. Upatikanaji wa majedwali ya kuangalia mwenendo wa kazi ulisaidia kwa kiasi kikubwa kufuatilia ubora wa kazi. Kazi ya uhariri wa taarifa za utafiti huu kwa hatua ya pili ilikamilika mwezi Oktoba 2022.

## MATOKEO MUHIMU

### KIWANGO CHA MWITIKIO

Jedwali Na.1 linaonesha kiwango cha mwitikio wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022. Jumla ya kaya 16,312 zilichaguliwa kwa ajili kushiriki katika Utafiti wa TDHS-MIS 2022. Idadi hii ya kaya ni pungufu kidogo ya kaya 16,354 zilizotarajiwa kushiriki na hii inatokana na eneo moja la kuhesabia watu kuwa na changamoto za kiusalama na maeneo mengine machache kuwa na kaya chache kuliko kaya 26 zilizokuwa zichaguliwe katika kila eneo la kuhesabia watu lililokuwa limechaguliwa kwa ajili ya utafiti kama ilivyokuwa imeainishwa wakati wa kuandaa sampuli. Kwa maeneo ya kuhesabia watu yaliyokuwa na kaya chache, kaya zote zilichaguliwa kushiriki kwenye utafiti. Kati ya kaya 16,312 zilizochaguliwa kushiriki katika utafiti, kaya 15,907 zilikutwa zinakaliwa na watu. Kati ya kaya zilizokuwazinakaliwa na watu, kaya 15,705 zilishiriki na kukamilisha mahojiano kikamilifu na hivyo kupelekea kiwango cha mwitikio kuwa asilimia 99. Katika kaya zilizohojiwa, jumla ya wanawake 15,699 walibainika kuwa na sifa (waliokuwa na umri wa miaka 15-49) za kufanyiwa mahojiano binafsi. Kati ya wanawake waliokuwa na sifa za kuhojiwa, wanawake 15,245 walikamilisha mahojiano binafsi na kupelekea kiwango cha mwitikio wa asilimia 97. Katika sampuli ndogo ya kaya zilizochaguliwa kwa ajili ya utafiti wa wanaume, wanaume 6,367 walibainika kuwa na sifa

(wenye umri wa miaka 15-49) za kushiriki katika Utafiti wa mtu binafsi na wanaume 5,763 walihojiwa kwa ukamilifu na kupelekea kiwango cha mwitikio wa asilimia 91.

<b>Jedwali Na. 1: Matokeo ya Mahojiano ya Kaya na ya Mtu binafsi</b>					
<b>Idadi ya kaya, wahojiwa, na kiwango cha mwitikio, kulingana na makazi, Tanzania DHS-MIS 2022</b>					
<b>Matokeo</b>	<b>Tanzania Bara</b>			<b>Zanzibar</b>	<b>Tanzania</b>
	<b>Mjini</b>	<b>Kijijini</b>	<b>Jumla</b>		
<b>Mahojiano ya Kaya</b>					
<b>Kaya zilizochaguliwa</b>	4,763	9,201	13,964	2,348	16,354
<b>Kaya zilizokuwa na watu</b>	4,587	9,019	13,606	2,301	15,907
<b>Kaya zilizohojiwa</b>	4,493	8,957	13,450	2,255	15,705
<b>Kiwango cha mwitikio wa kaya<sup>1</sup></b>	98.0	99.3	98.9	98.0	98.7
<b>Mahojiano na wanawake wenye umri wa miaka 15–49</b>					
<b>Idadi ya wanawake wanaostahili kuhojiwa</b>	4,741	8,345	13,086	2,613	15,699
<b>Idadi ya Wanawake waliohojiwa</b>	4,576	8,110	12,686	2,568	15,254
<b>Kiwango cha mwitikio kwa wanawake wanaostahili<sup>2</sup></b>	96.5	97.2	96.9	98.3	97.2
<b>Mahojiano ya kaya katika sampuli ndogo</b>					
<b>Kaya zilizochaguliwa</b>	2,382	4,600	6,982	1,170	8,177
<b>Kaya zilizokuwa na watu</b>	2,288	4,502	6,790	1,147	7,937
<b>Kaya zilizohojiwa</b>	2,232	4,469	6,701	1,129	7,830
<b>Kiwango cha mwitikio wa kaya katika sampuli ndogo<sup>1</sup></b>	97.6	99.3	98.7	98.4	98.7
<b>Mahojiano na wanaume wenye umri wa miaka 15–49</b>					
<b>Idadi ya wanaume waliostahili kuhojiwa</b>	1,788	3,545	5,333	1,034	6,367
<b>Idadi ya wanaume waliohojiwa</b>	1,547	3,225	4,772	991	5,763
<b>Kiwango cha mwitikio kwa wanaume wanaostahili<sup>2</sup></b>	86.5	91.0	89.5	95.8	90.5

<sup>1</sup>Kaya zilizohojiwa/Kaya zilizokuwa na watu  
<sup>2</sup>Wanakaya Waliohojiwa/ Wahojiwa waliostahili kuhojiwa

## SIFA ZA WAHOJIWA

**Jedwali Na. 2** linaonesha idadi na asilimia ya wanawake na wanaume waliohojiwa katika Utafiti wa TDHS-MIS 2022 kulingana na sifa zao. Matokeo yaliyowasilishwa katika ripoti ni wakilishi katika ngazi ya nchi, makazi ya mjini na kijijini, na kwa kila mkoa kwa mikoa yote 31 ya Tanzania.

- a) Takribani theluthi moja ya watanzania wanaishi maeneo ya mjini (asilimia 36 ya wanawake na asilimia 34 ya wanaume).
- b) Asilimia 16 ya wanawake Tanzania hawajasoma ikilinganishwa na asilimia 10 ya wanaume.
- c) Asilimia 72 ya wanawake na wanaume walisema afya zao ni nzuri au nzuri sana.
- d) Asilimia 27 ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 hawajawahi kuolewa ikilinganishwa na asilimia 44 ya wanaume ambao hawajawahi kuoia.
- e) Asilimia 61 ya wanawake na asilimia 51 ya wanaume wameoa/kuolewa au kuishi pamoja kama vile wameoana.
- f) Asilimia 20 ya wahojiwa wanawake na robo ya wahojiwa wanaume ni vijana wenye umri wa miaka 15-19.

Jedwali Na. 2: Sifa bainifu za wahojiwa						
Mgawanyo wa wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-49 kwa asilimia, kulingana na baadhi ya sifa bainifu zilizochaguliwa, Tanzania DHS-MIS 2022.						
Sifa Bainifu	Wanawake			Wanaume		
	Asilimia ya Watu (Weighted)	Idadi ya Watu (Weighted)	Sampuli ya watu (Unweighted)	Asilimia ya Watu (Weighted)	Idadi ya Watu (Weighted)	Idadi ya watu (Unweighted)
<b>Umri</b>						
15-19	20.2	3,083	3,142	25.1	1,444	1,457
20-24	17.9	2,727	2,710	16.2	934	959
25-29	16.6	2,533	2,500	14.8	850	846
30-34	13.6	2,076	2,041	13.3	765	722
35-39	12.4	1,884	1,882	12.0	693	686
40-44	10.4	1,588	1,550	10.5	607	621
45-49	8.9	1,363	1,429	8.1	469	472
<b>Hali ya afya kwa mujibu wa mhojiwa</b>						
Nzuri sana	17.9	2,726	3,105	22.6	1,303	1,446
Nzuri	54.1	8,254	8,042	49.8	2,872	2,890
Wastani	26.9	4,101	3,956	26.1	1,505	1,345
Mbaya	1.1	170	147	1.4	79	80
Mbaya sana	0.0	3	4	0.0	3	2
<b>Hali ya Ndoa</b>						
Hawajaolewa/hawajaoa	26.5	4,047	4,232	43.7	2,517	2,573
Wameoa/Wameolewa	43.5	6,630	6,751	45.5	2,621	2,539
Wanaishi Pamoja	17.2	2,622	2,400	5.5	316	346
Wameachana/Wametengana	10.4	1,585	1,514	4.9	280	287
Wajane/Wagane	2.4	370	357	0.5	28	18
<b>Makazi</b>						
Mjini	35.7	5,446	5,441	33.6	1,938	1,883
Kijijini	64.3	9,808	9,813	66.4	3,825	3,880
<b>Tanzania Bara/Zanzibar</b>						
Tanzania Bara	96.6	14,737	12,686	96.7	5,572	4,772
Mjini	34.5	5,268	4,576	32.5	1,871	1,547
Kijijini	62.1	9,468	8,110	64.2	3,700	3,225
Zanzibar	3.4	517	2,568	3.3	191	991
Unguja	2.5	381	1,566	2.5	143	625
Pemba	0.9	137	1,002	0.8	48	366
<b>Kanda</b>						
Magharibi	8.3	1,268	1,127	8.7	501	449
Kaskazini	11.4	1,733	1,461	10.9	631	470
Kati	10.3	1,573	1,328	10.0	577	489
Nyanda za Juu Kusini	6.1	924	1,209	6.5	376	474
Kusini	5.3	805	794	5.0	290	308
Nyanda za Juu Kusini Magharibi	8.7	1,322	1,767	9.1	526	725
Ziwa	29.2	4,454	3,148	29.4	1,694	1,255
Mashariki	17.4	2,657	1,852	16.9	976	602
Zanzibar	3.4	517	2,568	3.3	191	991
<b>Mikoa</b>						
Dodoma	5.1	772	463	4.4	255	157
Arusha	3.7	558	545	3.5	202	168
Kilimanjaro	2.7	417	399	3.0	171	138
Tanga	5.0	758	517	4.5	258	164
Morogoro	4.8	727	538	4.8	274	192
Pwani	3.5	539	479	3.1	180	139
Dar es Salaam	9.1	1,391	835	9.1	522	271
Lindi	2.2	336	362	2.2	128	147
Mtwara	3.1	468	432	2.8	162	161
Ruvuma	2.5	382	456	2.9	167	206



**Jedwali Na. 2: Sifa bainifu za wahojiwa**

Mgawanyo wa wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-49 kwa asilimia, kulingana na baadhi ya sifa bainifu zilizochaguliwa, Tanzania DHS-MIS 2022.

Sifa Bainifu	Wanawake			Wanaume		
